

## Zalisha kwa malengo ili kupanua kilimo biashara



Picha: MkM

**Kama kawaida jarida hili linatoa wito kwa wakulima kuanzisha na kujenga kilimo kuwa biashara inayoweza kuleta faida na kukidhi mahitaji ya kila siku hapo nyumbani. Hata hivyo, imekuwa ni kawaida kwa wakulima wengi kufanya shughuli zao bila kufanya maandalizi thabiti, na bila kuwa na mipango itakayowawezesha kupanua uzalishaji na kuifanya kuwa endelevu.**

Swala hili ni kikwazo kikubwa sana kwa sababu hautaweza kufanya kazi zako kwa malengo unayoyajua, kuelewa na uliyoyaweka tangu mwanzoni. Utakuwa mtu wa kuchukua kila linalokuja mbele yako, na mwishowe unajikuta haujaweza kufanya jambo la maendeleo na kutokufikia malengo pia.

Kama haukufanikiwa kuyafikia malengo yako mwaka huu, usikate tamaa. Kuna msemu usemao tunajifunza kutokana na makosa, hivyo, kuna nafasi katika mwaka

unaokuja ya kuibua mipango yako, kuyafanyia kazi na kupata mafanikio mazuri. Na kama umefanikiwa mwaka huu, utatia fora zaidi ikiwa utayarekebisha makosa madogo yaliyokupata na kuyaimarisha yaliyokuletea fanaka.

Ni vyema sasa kujipanga na kufanya maandalizi: kuwa ni kilimo cha namna gani utafanya, ni ufugaji wa namna gani unaotaka kufanya, na ni nini malengo yako katika uzalishaji na uuzaji ili kupata bei inayofaa sokoni?

Mkulima Mbunifu linaendelea kuhakikisha kuwa linakusaidia kupata taarifa muhimu kwa kile ambacho umekusudia kufanya, iwe ni kulima au kufuga, pamoja na kukuhimiza kuingia katika usindikaji wa mazao utakayozalisha. Ikiwa hauna wazo la kile unataka kufanya basi soma yaliyomo kwenye jarida hili na bila shaka utapata wasaha kutokana na mafanikio ya wakulima wengine na uhitaji uliopo kwa watumiaji ya mazao ya kilimo.

### Yaliyomo

Kilimo ikolojia na vita ya umaskini	2
Kula vizuri upate nguvu ya kufanya kazi	6



MkM ni suluhisho kwa wakulima	8
MkM maswali na majibu	12

### Mpendwa Mkulima

Hongera kwa kufikia mwezi wa mwisho wa mwaka 2024. Niwapongeze sana wale ambao mmekua waadilifu kufatilia mafunzo katika nakala hizi kila zinapotoka. Sisi wengine tujifunze kupitia wao kwani hakuna kinachoshindikana.

Tunapomaliza mwaka wa 2024, tungependa kuwashauri wakulima kuendelea kuweka bidii zaidi katika uzalishaji na kujipatia swala la masoko mtazamo mpya. Tafuta soko kuliko wakati mwingine wowote. Hii ni kwa sababu soko ni muhimu sana katika uwekezaji na shughuli za kilimo kibiashara.

Hakikisha kuwa unajipanga kusindika mazao yako yatakayotokana na mimea na mifugo. Kwa ukweli, mkulima ambaye anapanda mazao yake akiwa hajui atauza wapi, anapanga kufeli au kupata hasara.

Ni muhimu kushirikishana na wakulima wengine wanaozalisha ama kufuga kama wewe, ujifunze kutoka kwao na wao pia wajifunze kutoka kwako. Wakulima ambao wamepata manufaa zaidi wanaweza kuwa msaada wa karibu katika kukufanya uweze kutekeleza mipango yako na kukumbana na changamoto unazopata shambani.

Mwisho, tunawashukuru wote kwa ushirikiano mkubwa hasa wafadhili wetu Biovision Foundation, Biovision Africa Trust (BvAT) na mshirika wetu Sustainable Agriculture Tanzania (SAT). Tunawatakia kheri na fanaka katika msimu huu wa sikukuu za mwisho wa mwaka na mwaka mpya ujao wa 2025.

Endelea kufatilia Mkulima Mbunifu kwa kilimo chenye tija!



+255 717 266 007  
[http://www.facebook.com/mkulima\\_mbunifu](http://www.facebook.com/mkulima_mbunifu)  
[http://twitter.com/mkulima\\_mbunifu](http://twitter.com/mkulima_mbunifu)  
[https://www.instagram.com/mkulima\\_mbunifu](https://www.instagram.com/mkulima_mbunifu)  
[mkulimambunifu.org](http://mkulimambunifu.org)  
[theorganicfarmer.org](http://theorganicfarmer.org)  
[infont-biovision.org](http://infont-biovision.org)

Wasiliana na MkM,  
 S. L. P 14402, Arusha,  
 Simu: 0717 266 007, 0762 333 876,  
 Barua pepe:  
[info@mkulimambunifu.org](mailto:info@mkulimambunifu.org)  
[www.mkulimambunifu.org](http://www.mkulimambunifu.org)

# Kilimo ikolojia kinawezekana kupiga vita umaskini

**Katika kijiji cha Oldonyowas, wilaya ya Arusha, ambako kilimo kimekuwa shughuli kuu ya jamii kwa muda mrefu, Flora Godson (43) ni mfano bora kuonyesha ni jinsi gani dhamira na fikra bunifu inaweza kutimia.**


**Emmanuel Kasembe**

Safari yake kutoka kuwa mkulima mdogo hadi kuwa 'Mkulima wa Kwanza wa Mwaka kwa Wilaya ya Arusha' ni uthibitisho tosha wa nguvu ya mabadiliko ya kilimo ikolojia. Kilimo hiki sio tu kizuri kwa kudumisha mazingira bali pia huboresha maisha.

## Mwanzo

Hadithi ya Flora Godson ilianza kwa uamuzi wa kijasiri wa kubadili kilimo chake kwenda kwenye kilimo ikolojia mara baada ya kujiunga na kikundi cha Shifura, moja ya vikundi vinavyoingwa mkono na Mpango wa Kilimo Endelevu Arusha. Mpango huo ulikuza kilimo cha ikolojia kama kilimo ambacho kinasisitiza usawa wa ikolojia, uhifadhi wa bioanuwai na kupunguza utegemezi wa pembejeo za kemikali za viwandani.

Licha ya mashaka ya awali kutoka kwa majirani zake na changamoto alizokumbana nazo kama vile uhaba wa maji, ukosefu wa rutuba kwenye udongo na soko lisilo imara la mazao ya shambani, Flora alidhamiria kufanya mabadiliko hayo. Alianza kwa kubadilisha shamba lake kwa kujumuisha aina mbalimbali za



Picha: IDP

mboga, kunde na mazao ya matunda. Kupitia kujifunza kwa vitendo, aliweza kujumuisha mbinu tofauti kama vile kutengeneza mboji, dawa ya kuulia wadudu, uzalishaji wa mbolea ya mimea na mzunguko wa mazao, pia aliweza kuhuisha ardhi yake. Baada ya muda, shamba lake lilibadilika na kuwa mfumo wa ikolojia unaostawi, ambapo bayoanuwai ilitawi na udhibiti wa wadudu wa asili ukakita mizizi.

## Changamoto

Njia ya mafanikio haikuwa rahisi, Bi. Flora alikabiliwa na upinzani kutoka kwa wakulima jirani ambao walisita kubadilika na kuacha njia yao ya kilimo ya kawaida tu. Zaidi ya hayo, mavuno yake ya awali yalikuwa ya chini kuliko ilivyotarajiwa jambo ambalo lilitilia shaka ufanisi wa mbinu za kilimo ikolojia katika jamii. Walakini, ahadi yake haikuyumba. Aliendelea kujifunza, kurekebisha na kuboresha mazoea yake na hatimaye, matokeo yakaanza kujieleza yenyewe.

## Mafanikio

Udongo umeongeza rutuba zaidi, mazao yake yanastahimili ukame na hayana kemikali yeyote. Sasa ameanza kupokea wanunuzi zaidi na kupata bei nzuri katika masoko ya ndani. Shamba la Flora si chanzo cha chakula tena limekuwa kielelezo cha uendelevu na ustahimilivu wa kiuchumi katika jamii yake.

Shamba la Flora limepata uangalizi kwa haraka zaidi ya kijiji chake huku maafisa kilimo, wakulima wenzake na wadau mbalimbali wakianza kutembelea ili kujifunza kutokana na mazoea yake. Amekuwa mshauri na kuhimiza wengine kukumbatia kilimo ikolojia.

Kujitolea kwake katika kilimo kumemwezesha kuchaguliwa kushiriki mashindano ya kilimo ya wilaya, ambapo aliibuka kuwa "Mkulima wa Kwanza wa Mwaka kwa Wilaya ya Arusha". Waamuzi walivutiwa na



Picha: IDP

utofauti wa shamba lake, urejelezaji wa rasilimali, tija kwa kila eneo na mbinu bunifu anazotumia.

## Kuchochea mabadiliko

Mafanikio ya Flora ni zaidi ya mafanikio binafsi, ni kielelezo chenye nguvu cha uwezo wa kilimo ikolojia kubadilisha kilimo si kwa Tanzania pekee mbali duniani kote. Hadithi yake ni wito wa kuchukua hatua kwa wakulima, watunga sera na jamii kufikiria upya mbinu zao za kilimo. Kilimo ikolojia inatoa njia ya kuongezeka kwa mavuno, uendelevu wa mazingira na uthabiti wa kiuchumi. Ni mbinu ya kilimo ambayo inalinda maliasili zetu huku ikitupa chakula chenye lishe bora na kuboresha maisha yetu.

Yeye ni uthibitisho kwamba kilimo ikolojia sio tu mbadala unaofaa mbali ni mbinu muhimu kwa siku zijazo za kilimo. Kwa kukumbatia kilimo ikolojia, tunaweza kujenga mfumo endelevu wa kilimo na chakula ambao unasaidia afya ya dunia na ustawi wa jamii zetu.

Safari ya Flora ni mwanga wa matumaini, inayoonyesha kuwa wakulima wanaweza kustawi huku wakilinda mazingira, kujitolea na kupata usaidizi unaofaa. Mafanikio yake katika Wilaya ya Arusha ni ujumbe kwa ulimwengu kuwa uzalishaji wa kilimo ikolojia kinafanya kazi na ni mustakabali wa kilimo.

Mkulima Mbunifu ni jarida huru kwa jamii ya wakulima Afrika Mashariki. Jarida hili linaenea habari za kilimo hai na kuruhusu majadiliano katika Nyanja zote za kilimo endelevu. Jarida hili linatayarishwa na *Mkulima Mbunifu*, Arusha, ni mojawapo ya mradi wa mawasiliano ya wakulima unaotekelezwa na Biovision ([www.biovision.ch](http://www.biovision.ch)) kwa ushirikiano na Sustainable Agriculture Tanzania (SAT), ([www.kilimo.org](http://www.kilimo.org)), Morogoro. Jarida hili linafadhiliwa na Biovision Foundation



**Wachapishaji:** African Insect Science for Food and Health (ICIPE), S.L.P 30772 – 00100 Nairobi, Kenya, Simu: +254 20 863 2000, [icipe@icipe.org](mailto:icipe@icipe.org), [www.icipe.org](http://www.icipe.org)

**Mpangilio:** Cathbert Msemu 0757 847 481

**Mhariri:** Erica Rugabandana

**Mhariri Msaidizi:** Flora Laanyuni

**Anuani:** *Mkulima Mbunifu*

Sakina, Majengo road, (Elerai Construction Block)

S.L.P 14402, Arusha, Tanzania

Ujumbe mfupi pekee: 0785 496 036, 0766 841 366

Piga simu: 0717 266 007, 0762 333 876

Barua pepe: [info@mkulimambunifu.org](mailto:info@mkulimambunifu.org)

[www.mkulimambunifu.org](http://www.mkulimambunifu.org)



# Wakulima waungana kufanikisha mradi wa ufugaji wa kuku

*Umoja ni nguvu na wakulima wanapoungana pamoja, mambo mazuri hufanyika. Wanatiana nguvu, kuleta rasilimali pamoja na kuanzisha miradi ambayo ni ngumu kwa mkulima mmoja kuanzisha.*

## Eliudi Letungaa

Kikundi cha Shangushangu kilichopo kijiji cha Narunyu, kata ya Tandangongo, mkoani Lindi lina wanachama 16 (wanawake 8 na wanaume 8) na kilianzishwa mwezi wa saba mwaka 2023 likiwa na lengo la kujifunza kilimo na ufugaji kwa mbinu bora za kilimo hai.

Wanachama wote wa kikundi hiki wanatoka katika kijiji cha Narunyu, na walipata hamasa ya kuunda kikundi baada ya kupata uelewa wa kilimo hai kutoka Mkulima Mbunifu, hasa kuhusu kubadilisha mkondo na kupunguza na kuzalisha bidhaa za kilimo na mifugo zisizokuwa na viambata sumu ili kuimarisha afya ya walaji. Pia, wanachama waliona urahisi wa utekelezaji wa aina hii ya kilimo kwa kuwa asilimia kubwa kinatumia malighafi zinazopatikana shambani na zinazomzunguka, na kwa kufanya hivi mkulima anapunguza gharama za uzalishaji. Hii inamaanisha kwamba mkulima anazalisha chakula salama kwa gharama ya chini na kujiongezea kipato.



## Shughuli za kikundi

Kikundi hiki kinajihusisha na ufugaji wa kuku na kilimo cha mazao ya msimu kama mahindi, mbaazi, ufuta, alizeti na mikunde. Kuku wanafugwa katika banda la kikundi lililojengwa kwa nguvu zao wenyewe na walianza na kuku 100. Kuku hawa walipokomaa, waliuzwa na fedha zilizopatikana ziliweza kutumika kununua kuku wengine, wakiongeza idadi na kufikia kuku 200.

## Misingi ya kilimo hai

Mfumo wa ulishaji unaotumika ni kulisha vyakula maalumu kwa muda



wa wiki nne kisha kutengeneza mchanganyiko kwa kutumia malighafi zinazopatikana katika mazingira ya wafugaji kama vile mbaazi, kunde, mashudu ya alizeti, mahindi na kadhalika.

Kwa upande wa magonjwa, wanatumia dawa za asili kama vile kitunguu saumu, tangawizi, majani ya mpapai, mlonge, na chanjo kwa magonjwa hatari kama vile kideri.

## Malengo ya kikundi

- Kufikisha kuku 500 ifikapo Disemba 2025.
- Kila mwanakikundi kumiliki mradi wa ufugaji wa kuku 100 kufikia mwaka 2027.
- Kuanzisha kilimo cha bustani kitakachosaidia uchumi wa kikundi pamoja na uhakika wa upatikanaji wa mboga mboga kwa kuku na matumizi ya nyumbani.

## Dawa za asili kwa kuku

- Urahisi wa upatikanaji kwa kuwa dawa zinazotumika zipo katika mazingira ya wafugaji.
- Urahisi katika maandalizi na usalama kwa kuwa si hatarishi kwa afya ya kuku na binadamu.
- Mbali na kutumika kama tiba, hutumika kama sehemu ya lishe. Mfano, tangawizi hutumika kama tiba dhidi ya mafua ya kuku na ni chanzo cha Vitamin C ambayo ni muhimu kwa kuhimarisha kinga ya mwili ya kuku. Majani ya mpapai ni chanzo cha Vitamin muhimu hasa nyakati za kiangazi ambapo



asilimia kubwa ya nyasi huwa zimekauka.

## Faida kutokana na Mkulima Mbunifu

- Jamii imepata hamasa na uelewa kuwa kuku wanaweza kufugwa kwa njia za asili na kupata matokeo chanya.
- Kikundi kimetengeneza ajira kwa jamii, mfano, huwa wanunua malighafi mbalimbali za kutengeneza chakula cha kuku. Wanunua makaa kwa ajili ya kupasha joto vifaranga. Pia, kuna wanunuzi wa kuku ambao wanaenda kukaanga na kuuza vipande kwa wateja wao. Kwa kufanya hivyo, wanaunda nafasi za biashara na kwa wanajamii wanaojipatia kipato.
- Mradi umekuwa ni chanzo cha kupata mbolea ya uhakika isiyokuwa na viambata sumu kwa wakulima wa bustani. Baada ya kumaliza mzunguko wa uzalishaji (baada ya kuuza kuku), maandazo huondolewa na kutumika kama mbolea shambani.
- Kupitia mradi huu lishe kwa wanajamii imeimarika kwa kuwa kuku na mayai ni chanzo kizuri cha protini inayohitajika kwa ukuaji bora wa mwili.



## Faida kiuchumi

Kupitia mradi huu, kikundi kimepata fedha kwani mwezi wa Mei mwaka huu walifainikiwa kuuza jumla ya kuku 99 na hela TShs 1,323,000, faida ikiwa TShs 500,000. Hii ni baada ya kuondoa gharama zote za uzalishaji. Faida hiyo imewawezesha kuongeza idadi ya kuku na kuendelea kupanua mradi.

**Kwa mawasiliano na kikundi hiki cha Shangushangu kupitia John Cosmas Ng'habi kwa simu 0689081581 au barua Pepe: [johncosmasnghabi@gmail.com](mailto:johncosmasnghabi@gmail.com) / [cosmasjohn@gmail.com](mailto:cosmasjohn@gmail.com).**



# Kilimo ikolojia kimeniongezea tija katika uzalishaji

*Mbegu bora ya asili huchangia pakubwa katika usalama wa chakula na lishe kwa familia na jamii kwa ujumla. Hii inaambatana na matumizi ya mbinu bora za kilimo endelevu ili kumhakikishia mkulima uzalishaji wa juu nyakati zote na kwa muda mrefu.*

## Daudi Manongi

“Kabla ya kushiriki katika mradi wa CROPS4HD (Mazao yenye afya yasiyopewa kipaumbele), Mama Regina Mrope, kutoka Kijiji cha Mpindimbi, Masasi, Mkoani Mtwara, alikumbana na changamoto nyingi katika uzalishaji. Alikuwa akifanya kilimo cha mazoea akizalisha mazao ya asili yasiyotoa mavuno mengi huku akikosa mbegu bora na kutumia mbinu finyu za kilimo.

Hata hivyo, maisha ya Mama Regina yalibadilika baada ya kuwa moja ya wanufaika wa mradi wa CROPS4HD, ambao ulilenga katika utafiti na maendeleo, ikiwemo mbegu za mikunde ya Bambara kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania. Badala ya kutegemea mbegu bora pekee, mradi huu ulilenga mbegu ambazo zimezoleka kwa wakulima na huendana na mazingira ya kila eneo. Mradi ulimpa Mama Regina mafunzo na rasilimali za jinsi ya kusimamia na kuzalisha mbegu hizi za asili kwa ubora zaidi, ikiwemo njugu Myeupe-1, Tanbam, Mnyao mkubwa, Nalbam 4, njugu nnyeupe-2, Ifunda, na Bahi nyeupe.

Mama Regina anasema kuwa mafunzo haya yalimsaidia kupata ujuzi mpya katika uteuzi na uchaguzi wa mbegu, kuzalisha mbegu, na mbinu bora za kilimo endelevu. Kwa kutumia ujuzi huu, aliboresha



Picha: TABIO

kilimo katika shamba lake na kuwa msimamizi wa mbegu katika jamii yake. Moja ya majukumu yake ni kuhakikisha mbegu hizi za kipekee zinahifadhiwa na zinapatikana kwa wakulima wengine.

## Mafanikio ya bahi nyeupe

Miongoni mwa aina za mbegu alizotumia ni Bahi nyeupe ambayo ni nzuri kwa ladha na ina uwezo wa kustahimili mazingira mbalimbali. Aina hii ya mbegu ilifanya vizuri katika ardhi yake na kuleta mavuno mengi. Kwa sasa, mbegu hii ni maarufu kwa matumizi mbalimbali kama kupika ugali, chapati, na kuongezea ladha kwa mchele.

Mama Regina alifanikiwa kuuza yake ya ziada na kupata kipato cha ziada. Kwa mara ya kwanza, Mama Regina alipata fursa ya kipekee kuwekeza katika maendeleo ya shamba lake na kuboresha hali ya maisha ya familia yake kupitia faida hii ya kifedha.

Baada ya kuuza mazao yake Mama Regina alitumia kipato kupanua shughuli zake za kilimo kwa kununua ekari moja ya ardhi (shamba) ambayo

amepanga kuitumia kwa kilimo cha mbegu za njugu na ulezi. Kuongezeka kwa eneo la shamba, kutamwezesha kulima mazao mengi kwa manufaa ya familia yake na kwa ajili ya kusambaza mbegu bora kwa jamii yake. Hii itasaidia kuongeza usalama wa chakula katika kijiji chake.

Baadaye, Mama Regina alipata nafasi ya kushiriki katika maonyesho ya chakula na mbegu (Siku ya Chakula Duniani) yaliyofanyika Kigoma na Bukoba. Maonyesho haya yalikuwa fursa muhimu kwa Mama Regina kuungana na wakulima kutoka mikoa mengine, kubadilishana maarifa na kuonyesha mbegu zao. Katika maonyesho haya, aliweza kuuza mbegu zake na kubadilishana mbegu na wakulima wengine, jambo ambalo lilipanua mtandao wake na kumjengea kujiamini zaidi.

Aidha, Mama Regina amekuwa msimamizi wa benki ya mbegu ya jamii, ambapo ana jukumu la kuhakikisha kuwa mbegu bora na za asili zinapatikana kwa wakulima wa Mpindimbi. Kwa kushirikiana na wakulima wengine, mama huyu ameweza kusaidia kuboresha mbinu za kilimo na kuongeza uzalishaji, hivyo kusaidia familia nyingi kuwa na chakula cha kutosha na cha lishe ya juu.

## Malengo ya siku za usoni

Mama Regina anaangalia mbele na kujikaza akiwa na matumaini ya mafanikio makubwa zaidi. Anapanga kuendelea kuzalisha zaidi mbegu za njugu mawe, kwa manufaa ya familia na jamii kwa ujumla. Kama kiongozi katika kilimo endelevu, bado anajitolea kutunza maarifa ya kilimo cha asili na kuyapitisha kwa wakulima wenzake na vizazi vijavyo.



Picha: TABIO



## Nimetatua changamoto za magonjwa kupitia habari na elimu

*Mkulima huyu anaeleza namna jarida la Mkulima Mbunifu limemuwezesha kuzalisha mboga za majani na kutumia dawa za asili katika kupambana na magonjwa na wadudu ambao mara nyingi ni changamoto katika kilimo cha mboga*

### Flora Laanyuni

“Mimi ni Bi. Esther M. Ndosi (65), mkulima na mfugaji, mkazi wa Karansi, wilaya ya Siha. Nimejishughulisha na kilimo tangu mwaka 1977.

Kuzalisha mazao na ufugaji ndiyo shughuli kuu katika shamba langu inayoniingizia kipato na kunisaidia kumudu gharama na mahitaji yote ya kimaisha. Sina ajira nyingine, nategemea kilimo, hivyo naongeza juhudi na ujuzi kila mara.

### Nilianza aje kilimo

Mimi ni mzaliwa wa wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro. Nilibahatika kuolewa na kupata mji wa kudumu wilaya ya Siha ambapo niko na eneo kubwa la shamba ambalo lilikuwa pori. Kutokana na kuwa ni lazima kutafuta mahitaji ya kila siku ya kifamilia, niliamua kugeuza lile pori kuwa eneo la uzalishaji, na nilianza kuzalisha kahawa, kuotesha parachichi na migomba ambayo mpaka sasa ni mazao makuu yanayonipatia kipato.

Niliongeza mazao ya mahindi na maharage, ambapo ninalima wakati wa msimu pekee kwa sababu sina maji ya kuweza kufanya kilimo cha umwagiliaji.



### Mafunzo na elimu

Nilianza kupokea na kusoma jarida la Mkulima Mbunifu mwaka 2022 kupitia MVIWAKI. Nilivutiwa sana kufuatilia na kusoma majarida haya hasa nilipokutana na taarifa za kilimo cha mbogamboga, namna ya kufanya katika eneo ndogo, kupambana na magonjwa na jinsi ya kutafuta masoko.



Baada ya kusoma kwa muda na kaelewa mambo, nilianza kuzalisha mbogamboga aina ya sukuma wiki, chainizi na mnafu kwa msimu wote wa mwaka. Hivyo, mboga zinapatikana kwa matumizi ya familia, pia kwa ajili ya kuuza.

Kupitia jarida hili, niliweza pia kujifunza kuhusu ufugaji wa kuku wa kienyeji kwa lengo la kujiongeza kipato, zaidi kupata nyama na mayai ili kuboresha afaya ya familia.

### Mbinu ninazotumia katika kilimo

Kwanza ninazalisha kwa kutumia mbinu za asili au kilimo ikolojia ikiwemo kilimo mesto; ninachanganya kahawa, migomba na parachichi, matumizi ya mbolea ya samadi, pamoja na kilimo cha mzunguko wa mazao. Ili kudhibiti wadudu na magonjwa, ninatumia dawa za asili kama mwarobaini, majivu na pilipili. Kuelewa mzunguko wa maisha ya wadudu inasaidia kuweka mikakati ya kuzuia mashambulizi. Pia, dawa asili haziwezi kuwadhuru wadudu marafiki ambao wanachangia kupunguza iadadi ya wadudu waharibifu shambani.

### Changamoto katika kilimo

Changamoto inayonisumbua sana katika uzalishaji ni ukame kwani kwa kiasi kikubwa ninategemea maji ya

mvua. Wakati wa ukame, ninatumia maji ya mto kumwagilia mimea, ingawa wakati wa jua kali ya muda mrefu, maji hupungua au kukosekana kabisa. Hii inadunisha uzalishaji wangu na kupunguza mapato.

### Ushauri kwa wakulima

Ninachowashauri wakulima na wafugaji wenzangu;

Moja, wasiache kusoma jarida la Mkulima Mbunifu kwa kuwa lina manufaa mengi, ijapokuwa mimi ni mdhaifu wa macho, najitahidi kulisoma kila ninapolipata au namuomba mjukuu wangu anisaidie kusoma.

Pili, wasiache kufanya kilimo ikolojia na kujishughulisha mara kwa mara katika uzalishaji ili kuweka afya zao sawa, kujikinga na magonjwa, kuzalisha chakula safi na salama, na kuuza ya ziada ili kupata pesa za kukimu mahitaji ya kila siku.”





# Kula vizuri upate nguvu ya kufanya kazi

**Chakula na lishe ni muhimu kwa afya ya binadamu, hasa wakulima wanaotumia nguvu kazi nyingi shambani. Wakati mwingi wakulima wanazalisha na kuza, wanasahau kwamba pia wao wanahitaji lishe bora ili kuwa na nguvu ya kuendelea kufanya kazi na kuhakikisha usalama wa chakula.**

**Monica Morrison**

Ili kuwa na lishe bora tunapaswa kula mlo kamili na wa kutosha. Unapotafuta na kutayarisha chakula, zingatia makundi sita ya chakula ikiambatana na mazoezi ya mwili ambayo ni msingi wa afya njema. Makundi haya ni; nafaka na mizizi yenye wanga, vyakula jamii ya mikunde, vyakula asili nyama, mbogamboga, matunda na mafuta.

Chakula cha nafaka ni chanzo cha wanga na nguvu mwilini. Vyakula asili ya nyama husaidia kujenga mwili kwa uwepo wa protini. Hii ni pamoja na vyakula jamii ya mikunde ambayo huwa ni chanzo cha protini ambayo hujenga mwili. Mbogamboga na matunda huwa na vitamin na madini ambayo hujenga kinga ya mwili dhidi ya magonjwa. Nayo mafuta huipa mwili joto.

## Zingatia haya

- Punguza kiasi ya mafuta kwenye chakula. Ingawa mafuta muhimu mwilini, yana yanahitajika kwa kiasi kidogo tu. Zaidi, tumia mafuta yatokanayo na mimea ikilinganishwa na mafuta inayotokana na mifugo.
- Ongeza matunda na mbogamboga kwa wingi. Hivi ni vyakula vyenye nyuzinyuzi ambayo husaidia katika usagaji wa chakula tumboni.
- Tumia chumvi iliyoongezwa madini joto (*iodine*), na utumie kwenye kupika vyakula kwa kiasi kidogo. Epuka kutoongeza chumvi ya ziada mezani wakati wa kula, ingawa inaongeza ladha kwa chakula, ukifanya hivi, utakula chumvi nyingi kupita kiasi.
- Sawa na chumvi, matumizi ya sukari yawe kwa kiasi kidogo. Punguza kula bidhaa zinazowekwa sukari, kwa mfano, biskuti, visheti, kashata, keki, pipi, chokoleti, jamu, na kadhalika. Vyakula aina tofauti huwa na sukari. Hivyo, tumia sukari ya dukani kwa kiasi kidogo. Unaweza kutumia asali kama



mbdala ya sukari, pia, kwa kiasi kidogo.

Hata hivyo, uaji bora unatakiwa kuzingatia mahitaji ya mwili kulingana na umri, kazi ama shughuli anazofanya mtu, na pia hali ya afya ya mtu.

## Watoto

Watoto chini ya miezi sita wapewe maziwa ya mama pekee, pasipo kutumia chakula kingine.

Watoto wenye umwri wa miezi sita hadi miaka miwili wapewe maziwa ya mama na chakula mchanganyiko cha nyongeza. Chakula hiki kitengenezwe kwa kutumia vyakula asili. Iwapo mtoto hanyonyi maziwa ya mama, anahitaji kupewa maziwa (baada ya mwaka mmoja) mengine (kama ya ng'ombe) angalau nusu lita kwa siku na chakula mchanganyiko.

Watoto wenye miaka miwili mpaka mitano wale angalau milo mitano kwa siku (kwa viwango vidogo-vidogo) na maziwa yaendeleo kuwa sehemu ya mlo wa mtoto.

Watoto wa miaka sita hadi tisa wapewe milo kamili mitatu na vitafunwa mara mbili au tatu kwa siku. Vitafunwa hivi visiwe na sukari au mafuta mengi.

## Vijana

Vijana (wavulana na wasichana) wanahitaji virutubishi kwa wingi zaidi kwani wanakua haraka, hivyo ni muhimu kuongeza kiasi cha chakula. Wasichana wanahitaji madini chuma kwa wingi kwa sababu hupoteza damu wakati wa hedhi, hivyo wale vyakula

vyenye madini chuma (*iron*), asidi ya foliki na vitamini C kwa wingi ili kutengeneza chembe chembe za damu kwa wingi. Inashauriwa pia watumie chumvi yenye madini joto (*iodine*).

## Wazee

Wanahitaji mlo kamili midogo-midogo mara nyingi kwa siku. Wale vyakula laini vyenye virutubishi kwa wingina vyakula vyenye madini ya chokaa (*Calcium*) kwa wingi kama maziwa na dagaa. Waongeze ulaji wa vyakula vyenye nyuzi-nyuzi ili kusaidia mfumo wa usagaji wa chakula.

## Mwanamke mjamzito

Mwanamke mjamzito anahitaji kuongeza chakula kukidhi mahitaji yake binafsi na ya mtoto aliye tumboni. Vinginevyo anaweza kupatwa na matatizo ya kiafya. Anapaswa kutumia vidonge vya madini chuma (*iron*), vidonge vya asidi ya foliki, vidonge vya kutibu minyoo, dawa za kuzuia malaria na alale ndani ya vyandarua vilivyowekwa viutilifu ili kijikinga dhidi ya mbu na malaria. Vyote hivyo ili kuzuia upungufu wa damu. Pia, atumie chumvi yenye madini joto (*iodine*).

## Mbinu asili

Wakati chakula kiko shambani ni muhimu sana kwa mkulima kutumia mbinu sahihi za kiasili ili kulinda afya ya kilichozaishwa na kutunza rutuba ya udongo. Hii ni pamoja na matumizi sahihi ya mbolea asili, madawa ya wadudu na dawa ya kukuzia (*booster*). Kumbuka kuwa bidhaa inayotoka shambani ikiwa na vimelea vya sumu vitaadhi usalama wa mtumiaji na kupunguza ubora wa chakula.

Wakati wa kuanda vyakula inabidi tuwe na umaakini ili tulinde ubora wa chakula husika. Hakikisha unaosha mboga za majani na kuacha zitoke maji kabla ya kukata. Pika mboga za majani kwa muda mfupi, na endapo utahitaji kuchemsha mboga, tumia maji kidogo na usiyamwage.



# Siku ya chakula duniani October 2024

*Siku ya chakula duniani ni maadhimisho ambayo yaliwaleta pamoja wadau wa kilimo na chakula kutoka sehemu mbalimbali. Hata hivyo siku hii ilikuja huku kukiwa na mvutano na mizozo ya kimataifa na majanga ya tabianchi ambayo ni miongoni mwa mambo yanayochangia changamoto ya mamia ya mamilioni ya watu duniani kote kukabiliwa na njaa na mabilioni ya watu kushindwa kumudu chakula bora.*

**Monica Michael Morrison**

Katika kuhakikisha lishe inakuwa jambo la msingi kwa wote katika maadhimisho ya siku ya chakula duniani mradi uliweza fanya maadhimisho haya kupitia chakula cha asili ambacho kilizingatia usalama wa vyakula na namna mbalimbali za uandaji wake kwa kujali ulindaji wa virutubishi.

Lishe husaidia ukuaji sahihi, na tunashauri matumizi ya bidhaa mbalimbali za asili ambazo ni safi na salama.

Matumizi mbali mbali ya vyakula ilikulinda afya na kuwa na lishe bora

Vyakula vingi vya asili vilivyotumika miaka ya nyuma vimekuwa na ubora wa kilishe na kulinda miili yetu na kutuinga na magonjwa mbali mbali. Hivi vyakula vimekuwa vikichanganywa na vitu mbalimbali;

- loshoro mchanganyiko wa mahindi na maziwa mgando (wanga na protini) na wengine huongeza aina ya ndizi maarufu Mkoani Arusha kwa jina la ndizi ng'ombe.



Picha: IDP

- Ngitalolo mahindi, maharage, maziwa na mboga za majani (wanga, protini na vitamini)
- Matoke ndizi, maharage, nyama (wanga, protini ya kutosha)
- Sharubati mbalimbali kama vile rosela, ubuyu, ukwaju
- Matumizi ya bidhaa kama kweme inayoaminika kama kiungo cha mboga (protini)

## Elimu ya uandaaji sahihi wa vyakula vya asili ni muhimu sana kwa mfano:

- Epuka kutengeneza loshoro itakayokaa muda mrefu sana kwenye kibuyu na kuendelea ongeza maziwa.
- Epuka kuloweka mahindi kwa muda mrefu na kutwaga kwa matumizi hii hupoteza nguvu na ubora wa wanga.

- Kuosha mahindi au maharage kwa kutumia magadi, hakikisha utayapika kwa kuongeza viungo au kutumia mboga za majani pembeni ili kurudisha virutubisho ulivyopoteza.

Ikumbukwe kuna baadhi ya vyakula hutumiwa sana nchini Tanzania kama vile ugali (sembe/dona), makande, chapati, mboga za majani

## Vyakula hivi vinaweza ongezwa thamani zaidi kwa kuongeza ubora

1. Ugali; tuache dhana ya kutumai ugali wa mahindi peke yake unaweza changanya mahindi na mbaazi/ njugu mawe/ boga. Hapa tunapata ongezeko la protini kwenye ugali wetu hata vitamini zingine kama B
2. Makande; tumezoea kuchanganya mahindi na maharage tu ila unaweza weka mahindi, maharage, mbaazi, njugu mawe, ngano na karanga pia na viungo kama karoti, kitungu na nyanya. Hapa tunakuwa na mlo kamili
3. Chapati; tumekuwa na tabia ya kupika kutumia ngano peke yake bali unaweza changanya na boga au kiasi lishe hii inasaidia kupata vitamini A zaidi
4. Mboga za majani; kwa mazoea zaidi huwa viungo kama karoti na kitungu huwekwa kwa kiasi kidogo ila tunaweza ongeza kiwango cha hivi viungo ilikuwa na mboga zenye kiwango kikubwa cha virutubisho.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na Afisa lishe kutoka shirika la Iles De Paix (IDP) Monica Michael Morrison.**



Picha: MKM

Picha: MKM



# Masomo kupitia jarida ni suluhisho la changamoto za wakulima

*“Mimi ni mkulima na mfugaji, Ninazalisha kwa misingi ya kilimo ikolojia. Situmii pembejeo sumu za viwandani kuanzia ninapootesha zao husika au kuanza uzalishaji wa mifugo yangu mpaka ninapovuna, kuhifadhi na kuuza mazao yangu.”*

## Juma Mchinja

Ninafanya uzalishaji wa mazao ya aina mbalimbali kama vile ndizi, kahawa, njugu, maharage, mahindi, mbogamboga, na pia ninafanya ufugaji wa kuku pamoja na mbuzi.”

Hayo ni maneo ya Bw. Deogratus Joseph (66) toka Kyaka, wilaya ya Misenyi mkoani Kagera, miongoni mwa wanufaika wa jarida la Mkulima Mbunifu kupitia FADECO radio.

Bw. Joseph anaeleza kuwa, tangu kuzaliwa kwake wamekuwa wakizalisha mazao mbalimbali ikiwemo mazao makuu ya ndizi na kahawa bila kutumia aina yeyote ya pembejeo zenye kemikali sumu za viwandani na wamekuwa wakipata faida kubwa kwani ardhi yao ina rutuba ya kutosha kuweza kuzalisha mazao yenye tija.

Hata hivyo, baada ya kuanza mji wake aliendeleza uzalishaji wa mazao mengine, pia kufanya ufugaji ambapo mpaka sasa anazalisha kwa misingi ya kilimo ikolojia kwenye eneo la ukubwa wa ekari 17.

## Kwa nini Mkulima Mbunifu?

“Nilibahatika kupata nakala za jarida la Mkulima Mbunifu kupitia kwa rafiki yangu Bw. Joseph Sekiku, Mkurugenzi wa FADECO radio, na nilipopitia nakala ya kwanza niliipenda sana kutokana na taarifa za uzalishaji zilizochapishwa kwani zinalenga kwa asilimia kubwa kumsaidia mkulima wa chini kufanya kilimo kwa njia sahihi na rahisi jambo tunalolifanya hapa Kagera.

Nilifurahi sana kujua kuwa kumbe changamoto zinazotupa hasa za magonjwa ya mifugo tunaweza kupambana nayo kwa njia za kiasili yaani kwa kutengeneza dawa zinazotokana na malighafi zilizopo katika maeneo yetu, tukawapa kuku na wakapona.”

## Uzalishaji kwa misingi ya kilimo ikolojia ukoje?

“Kutokana na kuwa ardhi yetu ina rutuba ya kutosha kulingana na njia ya uzalishaji tunayoifanya, tunapata mavuno mengi na hatujawahi kabisa kutumia sumu za kemikali katika maeneo yetu, hivyo uzalishaji huu ni



Picha: FADECO

faida kwa mkulima kwani gharama ni ya chini.”

Bw. Joseph anaongeza kuwa, wanapata chakula salama kwa ajili ya familia zao, pia kwa ajili ya kuuza na kujipatia fedha za kujikimu katika shughuli na miradi mingine ya kifamilia.

## Vipi kuhusu soko?

“Soko la mazao yote ni kubwa na linapatikana kwa urahisi, bei ni nzuri na rafiki kwa mkulima. Kwa mfano, kuku wa kienyeji wanatafutwa sana na hawatoshenzi kabisa soko hata wana Kagera wote wakizalisha kuku bado soko ni kubwa sana. Kwa sasa, tetea anauzwa kati ya TSh 20,000/- hadi TSh 25,000/- huku jogoo akifikisha hadi TSh 30,000/-.”

## Changamoto

Bw. Joseph anasema kuwa, changamoto wanayokumbana nayo ni ya magonjwa hasa ugonjwa wa kideri kwa kuku na kupe kwa mbuzi. Mwanzoni mifugo walikuwa wakiteketea kwa asilimia kubwa mpaka walipokutana na wataalamu waliowashauri kuwachanja mifugo kila mara lakini. Hata hivyo, kama Mkulima Mbunifu inaposhauri, kuna mbinu bora za asili za kupambana na magonjwa bila gharama kubwa na kwa ufanisi.

## Wito kwa Mkulima Mbunifu

Jarida la Mkulima Mbunifu linatoa elimu muhimu sana kwa wakulima na wafugaji. Wakulima ambao hawapokei jarida hili wanakosa kitu kikubwa. Ni ombi langu MkM kuhakikisha wanatanua wigo wa kusambaza majarida haya kwa wakulima wengi zaidi nchini kwa manufaa ya uzalishaji wa leo na wa vizazi vijavyo.



Picha: FADECO



# Mbolea ya BOKASHI inapambana na mbadiliko ya tabia-nchi

*Kutana na mkulima Giranta Giranta, kutoka kijiji cha Bungurere, kata ya Muriba, wilaya ya Tarime, mkoani Mara. Tulizungumza naye kuhusu mbinu za kilimo endelevu anazotumia shambani mwake.*

Erica Rugabandana

“Najishughulisha na kilimo mseto ambacho imenipa tija kubwa kwenye uzalishaji wa mahindi na maharage. Ninashirikiana na wakulima katika eneo langu na pamoja tumeansiha kikundi kinachijulikana kama Tabukomu”.

## Umekumbana na changamoto gani?

Rutuba ya udongo ilikuwa chini na wadudu na magonjwa yalikuwa yanasumbua sana kwenye mazao na kufanya mapato kuwa kidogo.



## Mlipata usaidizi gani?

Baada ya kufika mradi wetu wa ASILI B kupitia wawezeshaji wetu wa shirika la TABIO tulipewa mafunzo kuhusu mbinu za kupambana na mabadiliko ya tabia-nchi ikiwemo namna ya kupambana na upoteaji wa rutuba ya udongo, yaani jinsi ya kuongeza rutuba ya udongo ili kuongeza uzalishaji.



## Tumejifunza kutengeneza mbolea hai aina ya BOKASHI tukitumia malighafi yafuatayo:

Samadi (mifuko 7) – chanzo cha naitrojini na vijidudu, Maganda ya mpunga/mahindi (mifuko 7) – kusaidia muundo wa mbolea, Udongo wenye rutuba (mifuko 5) – chanzo cha vijidudu, Unga wa mkaa hai (mfuko 1) – hifadhi ya vijidudu, Pumba (mfuko 1) – chakula cha vijidudu, Molasi (lita 5) – chanzo cha nishati, Hamira (½ kg) – kuchochea uchachushaji, Madini (majivu), na Maji – yasiyo na klorini. Tunachangaya malighafi haya na kupata mbolea mzuri kwa udongo na mimea.

## Umepata mafanikio gani?

Kwa sasa nimeweza kuongeza mazoa ya mahindi na maharage kutoka kuvuna gunia 3 ya mahindi na gunia 1 ya maharagwe hadi kufikia magunia 9 ya mahindi na gunia 3 za maharage kwa ekari moja.

Pia, nimepunguza gharama za uzalishaji hasa kununua mbolea za viwandani, badala yake natumia BOKASHI kupandia na kukuzia mimea. Hivyo nimeongea kipato, nina uhakika wa chakula na lishe, nimeongea bioanuai na kutunza mazingira, na kutoa

elimu kwa jamii iliyonizunguka kuhusu ubora na matumizi ya mbolea hii.

## Ushauri kwa wakulima Wengine

- Wakulima watumie mbinu za kilimo mseto na kuachana na kilimo cha mazoea ili kuongeza tija.
- Tumia mbegu za asili ili kuongeza vyanzo vya virutubisho na kuepuka tatizo la utapia mlo na magonjwa yasiyo yakuambukiza yanayosababishwa na lishe duni.
- Mbegu za asili zinaweza kupambana na kustahimili athari za mabadiliko ya tabia-nchi.





# Nimesoma MkM na kupiga hatua katika uzalishaji

**Wakulima wengi wamenufaika kutokana na elimu ya bure inayotolewa kupitia jarida hili. Wanasoma na kufanyia majaribio mbinu mbalimbali zinazosimuliwa, uzoefu wa wakulima na watalamu wa kilimo endelevu.**

## Flora Laanyuni

“Tangu mwaka wa 2012, nimekuwa msomaji wa jarida la Mkulima Mbunifu (MkM) na nimepiga hatua kubwa katika uzalishaji”, hivyo ndivyo alivyoanza kujitanabaisha Bw. Godwin Kimaro kutoka Karansi, mkoani Kilimanjaro, alipotembelewa na mwandishi wa jarida hili kwa lengo la kufahamu ni kwa namna gani jarida la Mkulima Mbunifu limekuwa nyenzo katika uzalishaji wa mazao na wanyama kwa wakulima na wanufaika katika eneo hilo.

Bw. Godwin ambaye alionyesha furaha alipotembelewa, alitoa nakala mbalimbali za jarida ambazo amekuwa akipokea kuanzia mwaka 2012. Anasema kwamba amekuwa akizisoma na kuhifadhi, pia akitumia elimu hiyo kwa vitendo katika shughuli zake za uzalishaji. Anaendelea kwamba MkM ni kama darasa kwa wakulima na linajibu changamoto nyingi za wakulima, kwa mfano, kuanzia kuweka malengo ya uzalishaji mpaka kufika kujenga na kudumisha soko.

“Nilianza rasmi kilimo biashara mwaka 2015 huku nikizalisha maharagwe, mahindi, ndizi na mbogamboga. Ingawa kwa uchache, ninafuga ng’ombe, kuku na mbuzi ambao kwa hakika wamekuwa msaada mkubwa kwangu kifedha na kwa chakula kwa familia yangu”, anasimulia.

## Kabla ya mafunzo

“Mimi nilikuwa nafanya kilimo, japo kwa kiasi kidogo, lakini nilikuwa nafanya kilimo cha asili yaani natumia



Picha: MkM

mbegu za asili, mbolea za wanyama, hivyo sikuwahi kutumia kabisa mbinu za kisasa kama madawa, mbegu na mbolea katika kuzalisha”, anaeleza.

Anasema kwamba jarida la Mkulima Mbunifu limemsaidia kufahamu na kufanya kilimo ikolojia kwa ukubwa na kupata faida, hasa pale anapozalisha kwa gharama nafuu, kupata mavuno mengi na kufikia soko kwa urahisi.

“Kupitia jarida hili, nimejifunza kufanya kilimo cha matuta ambacho toka awali sikuwa nakifahamu kabisa. Nimejifunza kufanya kilimo cha mbogamboga kwa ukubwa na kwa njia ya kibiashara. Nimeweza kufahamu aina za malisho, namna ya kuzalisha, kulisha mifugo na namna ya kutengeneza na kutumia aina mbalimbali za dawa za asili”, Godwin anaeleza.

“Aidha, nimeweza kujifunza kuhusu ufugaji wa kuku wa asili na kuanza mradi huo. Nimejifunza namna ya kuwapa chanjo kutoka vifaranga wanapoanguliwa mpaka wanapokuwa kuku wakubwa, namna ya kuandaa na kulisha chakula cha kuku, kuweka na kutunza kumbukumbu za uzalishaji”, anaendelea kusimulia.

Bw. Kimaro anasema kuwa yeye pamoja na wanakijiji wengine waliweza kutibu mifugo yao kutokana na ugonjwa wa mapele ngozi mara baada ya kusoma makala kwenye jarida la Septemba 2015, na mpaka sasa wanawachanja mifugo wao kila mwaka na huo ugonjwa haupo tena.

## Kuhusu wakulima wengine

Wakulima wengi wanawazunguka ni wanufaika wa jarida kwa mara wanapokea kwenye kikundi chao, wanasoma, kubalishana mawazo, nakala linagusa moja kwa moja shughuli wanazofanya na linatatua changamoto zao hapo kwa hapo.

## Changamoto katika kilimo

“Kila penye faida, changamoto hazikosekani na changamoto kubwa ninayokumbana nayo ni ukame, hivyo imenilazimu kuchimba maji ardhini ambayo natumia katika uzalishaji na hunigharimu kuweka umeme kwa ajili ya kupandisha maji na kusambaza shambani”, analalama. Hata hivyo, mkulima huyu anapanda mazao yanyoweza kustahimili ukame ili kuendeleza uzalisha mwaka mzima.

## Wito kwa MkM

Bw. Godwin anasema, “Naomba sana wadau wa jarida hili kututembelea mara kwa mara, kwanza kujionea kazi tunazozifanya, lakini pia kushauriana mambo kadhaa yanayotusumbua shambani kwani kuna maswali mengine tunaona tungeweza kupatiwa majibu sahihi ikiwa mtu amejionea mwenyewe kwa macho kile tungependa kuuliza.”



Picha: MkM

## Wito kwa wakulima

“Ningependa kuwashauri wakulima wenzangu kupenda kujisomea jarida hili mara wanapopata, pia kuhifadhi nakala hizi kwa matumizi ya baadaye kwani mimi mpaka sasa nina nakala zangu zote tokea mwaka 2012. Mara kwa mara, narejelea kusoma pale ninapokuwa na uhitaji”, anamalizia.



Picha: MkM



## Jarida la Mkulima Mbunifu na vipindi vya redio vyachochea kuenea kwa kilimo endelevu

*Kuna njia mbalimbali za kusambaza habari kuhusu kilimo kwa wakulima wadogo ili elimu iwafikie wakati unaofaa na kuwasaidia kufanya maamuzi yatakayowaletea tija shambani. Vipindi vya redio na majarida ya Mkulima Mbunifu yanapotumiwa kwa pamoja hutoa nafasi nzuri kwa wakulima kujifunza na kufanyia majaribio mbinu mbali za kilimo.*

### Charles Kikoricho

Thomas Amas ni mzaliwa wa Kijiji cha Kinku, kata ya Mung'aa, halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, mkoa wa Singida. Ana umri wa miaka 47, ana mke mmoja na watoto watano (wa kike watatu na wa kiume wawili). Watoto wake wa kike wana elimu ya kidato cha nne na wa kiume wanaendelea na masomo ya shule ya msingi.

Thomas alianza shughuli za Kilimo akiwa mtoto mdogo kutokana na familia na jamii inayomzunguka, shughuli kuu ikiwa ni kilimo. Mwaka wa 2021, alianza kulima kwa msingi wa kiikolojia baada ya kupata elimu kwa kusoma jarida la Mkulima Mbunifu ambalo linachapisha mbinu na kanuni mbalimbali za kilimo cha kiikolojia. Hii ni pamoja na kusikiliza mfululizo wa vipindi vya redio vinavyorushwa na Standard Radio FM ya Singida ikishirikiana na Farm Radio International (FRI). Mbinu hizi ni kama vile matumizi ya mbolea ya mboji na samadi, dawa za asili za kuuwa madudu wanaoharibu mimea.

### Dawa asili

Thomas anasema kuwa hapo mwanzo alikuwa anatumia fedha nyingi kununua dawa za kuulia wadudu waharibifu kwenye mimea, kununua mbolea na mbegu, lakini baada ya kusoma makala na kusikiliza vipindi vya redio aligundua na kujua kwamba



zipo dawa za asili ambazo zinawua wadudu na ambazo zinapatikana bila kutumia fedha nyingi na vinasaidia chakula kutopata sumu yoyote inayoweza kuathiri afya ya walaji.

Madawa haya ni kama vile majivu, ndulele, mwarobaini na kadhalika. Aligundua kwamba jamii ya Ikungi imezoea kutumia mti unaitwa Mtuguru kudhibiti wadudu. Wanatwanga-twanga kisha kuloweka kwa maji kwa muda wa siku saba na inakuwa tayari kupulizia mimea.

### Kurutubisha udongo

Pia, yeye na wakulima wengine walijifunza kutengeneza mbolea ya mboji. Wanachimba shimo na kufukia takataka huku wananyunyizia maji juu ya shimo. Baada ya siku 14, wanageuza takataka ndani ya shimo. Wanaiacha ioze vizuri na itakuwa tayari kwa matumizi shambani. Kilimo mseto ni mbinu nyingine ambayo wanatumia katika mashamba yao. Hii ni kupanda mazao zaidi ya moja, mfano, kulima mahindi na Karanga au maharagwe katika eneo moja.

### Manufaa

Thomas anasema kuwa baada ya kuanza kulima kwa mtindo wa kilimo ikolojia, ameona faida nyingi ikiwemo kuondoa gharama za ununuaji wa pembejeo na viatilifu au dawa za wadudu waharibifu. Yeye ni mfugaji, hivyo anatumia mbolea ya samadi inayotokana na ufugaji wa ng'ombe na kutengeneza mbolea ya mboji kutokana na masalio au mabaki ya mimea shabani. Anaongeza kwamba kilimo ikolojia inatunza ardhi/udongo kwani wakulima wameacha kuchoma mabaki mazao shambani.

Anaendelea kusema kwamba kilimo ikolojia imekuwa msaada mkubwa kwake kwa kujikwamua kiuchumi. Analima ekari moja ya

mahindi na anapata kati ya gunia 16 hadi 25. Hii ni mafanikio makubwa kwake kwani anazalisha kwa gharama ya chini mno.

Anaongeza kwamba kilimo imemsaidia yeye na familia yake kupata chakula safi, salama na chenye afya. Pia, mauzo ya mazao yake yamemwezesha kununua ng'ombe na mashamba mengine ya kulima.

### Kushirikisha wakulima wengine

Juhudi zake katika kilimo ikolojia imefanya jamii inayomzunguka Bw. Thomas kutambua na kushabikia weledi wake. Kwa sasa, yeye hutoa elimu ya mbinu endelevu za kilimo kwa wakulima wanaomtembelea shambani mwake na pia wanaomualika kuwatembelea, wakiwa watu binafsi au vikundi vya wakulima. Wengi wamenufaika kutokana na ushauri wake na kupata mazao mengi yenye tija na, yasiyokuwa na mabaki ya kemikali.



Pia, ameanzisha kikundi ambacho mpaka sasa kina jumla ya wakulima 102 ambao tayari wameunda shamba darasa ili kuendelea kujifunza zaidi kuhusu kilimo ikolojia. Kikundi hiki kinahakikisha kwamba wanachama wamesoma kila toleo la Mkulima Mbunifu na kusikiliza vipindi vya Farm Radio International (FRI) kupitia Standard Radio FM ili kuendelea kuboresha uzalishaji wao.



# Sikiliza vipindi vya kilimo ikolojia

Kama ilivyo ada *Mkulima Mbunifu* imeendelea kushirikiana na wadau wengine kuhakikisha inakufikishia taarifa sahihi za kilimo hai. Kwa mantiki hiyo, usiache kusikiliza vipindi vya kilimo hai vinavyoletwa kwako na shirika la Farm Radio International kupitia stesheni mbalimbali za radio.



JINA LA RADIO	JINA LA KIPINDI	NAMBA YA KUBIPU	SIKU YA KIPINDI		MARUDIO YA KIPINDI	
			SIKU	MUDA	SIKU	MUDA
RADIO MWANGAZA	KILIMO NA MWANGAZA	784105727	IJUMAA	2:30-3:00 USIKU	JUMATATU	2:30-3:00 USIKU
RADIO STANDARD FM	KILIMO NA JAMII	784105733	JUMAMOSI	1:00-1:30 JIONI	JUMATANO	1:30-2:00 USIKU
RADIO UTUME FM	KILIMO NA MKULIMA	784105788	ALHAMISI	2:30-3:00 USIKU	JUMAPILI	1:00-1:30 JIONI
RADIO KICHEKO FM	KILIMO FURSA	784105718	ALHAMISI	08:15 MCHANA	IJUMAA	02:00 USIKU
RADIO LUMEN FM	SHAMBA DARASA	784105788	JUMAMOSI	2:00 USIKU	JUMAPILI	04:00 USIKU

## Maswali toka kwa wasomaji wa jarida la MkM mtandaoni

**Matalis Komba anauliza:** Je, ni dawa gani ya asili kwa ajili ya Kideri?

**Jibu toka Mkulima Mbunifu:** Asante sana kwa swali lako. Ili kutibu ugonjwa wa Kideri kwa dawa za asili, chukua majani 3-5 makubwa ya Shubiri mwitu, katakata na loweka ndani ya maji lita 10 kwa masaa 12 hadi 16. Kisha, wape kuku kwa siku 5 hadi 7. Mwaga dawa inayobaki baada hizo siku na utengeneza tena nyingine kwa muda wa siku 5 mpaka 7. Mchanganyiko huu husaidia kupambana na Kideri/mdondo, sotoka, homa ya matumbo (typhoid), mafua, pamoja na kipindupindu cha kuku.



**Mtizi James anauliza:** Ningependa kujua mahitaji ya chakula cha Nguruwe, hasa kwa makundi tofauti ya nguruwe.

**Jibu toka Mkulima Mbunifu:** Mahitaji ya chakula au ulishaji wa nguruwe huongezeka kulingana na ukuaji wake (umri). Uwiano huu ambao hutokana na mchanganyiko wa vyakula vyote (madini, wanga, protini na vitamini) hutakiwa kupewa nguruwe mara mbili kwa siku.


Mfano, wiki 8 hadi 12 anakula kilo 1, wiki 12 hadi 18 anakula kilo 1.5, wiki 18 hadi 23 anakula kilo 2, wiki 23 hadi 30 anakula kilo 3. Kiwango hichi ni kwa siku na unagawa mara mbili kwa siku, asubuhi na jioni



**Tumaini Charles:** Utengenezaji wa dawa mbalimbali iwe za mifugo au binadamu hutokea katika vyanzo mbalimbali kama mimea, bakteria, fangas na baadhi ya aina za wanyama. Je, ufugaji wa kuku kwa kutumia njia asili kwa kuwatibu na kuwakinga ni sehemu ya njia bora ya utunzaji wa kuku?

**Jibu toka Mkulima Mbunifu:** Asante kwa kuwa miongoni mwa wadau na wasomaji wa jarida letu la MkM. Ni sahihi kabisa kuwa ufugaji wa kuku kwa njia ya asili ikihusisha kinga/tiba ni njia bora ya ufugaji wa kuku, kwani ni njia;

1. Salama ambayo haitumii kemikali za viwandani ambazo ni sumu na ambazo baadaye inaweza kusababisha madhara kwa mlaji.
2. Yenye gharama na nafuu kwa mfugaji kwani hutumia malighafi zinazopatikana kwenye eneo lake.
3. Mojawapo yenye tija kwa mfugaji kwani uzalishaji wa kuku na gharama za utunzaji ni ndogo, hivyo mfugaji atakapouza kuku wake hupata pato kubwa akishatoa matumizi.
4. Inayojali uzalishaji kwa misingi ya kilimo hai.



**Bakari Shabani anauliza:** Nguruwe aliye na ugonjwa wa ukurutu anaweza kuogeshwa na dawa za kuogeshea ng'ombe.

**Jibu toka Mkulima Mbunifu:** Kama nguruwe wako ana ugonjwa wa ukurutu, ni muhimu pia kufahamu ni aina gani ya ukurutu kwani kuna aina mbalimbali za ugonjwa huu. Hii itakusaidia kujua namna ya kupambana kuepuka kupata ugonjwa huu tena mara utakapowatibu.

Kuna dawa zinazotumika kwa ajili ya kuogeshea, na dawa hizi ni zile ambazo zina kiini tete kitiwacho Amitraz kama vile TIXFIX, BAMITRAZ na TWIGATRAZ. Pia, ugonjwa huu unaweza kutibiwa kwa dawa za sindano, yaani dawa aina ya Ivermectin na kwa kuzingatia utaratibu kutoka kwa mtaalamu wa mifugo kwa sababu kila mnyama hupewa dozi tofauti na mwingine.

Ili kukinga nguruwe na ugonjwa huu, hakikisha unafanya usafi wa banda mara kwa mara, kuogesha mifugo kila wakati kulingana na utaratibu unaotolewa na wataalamu wa mifugo, kupulizia banda la mifugo dawa zenye Amitraz ili kuua utitiri.

Ikiwa umegundua kuna mnyama ameanza kuonyesha dalili za ugonjwa huu, mpatie tiba mapema ili kuwakinga wengine na ikiwezekana wapatie na wanyama wengine wote ambao bado hawaonyesha dalili hiyo.



mkulimambunifu.org  
theorganicfarmer.org  
infontet-biovision.org

+255 717 266 007  
[http://www.facebook.com/mkulima\\_mbunifu](http://www.facebook.com/mkulima_mbunifu)  
[http://twitter.com/mkulima\\_mbunifu](http://twitter.com/mkulima_mbunifu)  
[https://www.instagramu.com/mkulima\\_mbunifu](https://www.instagramu.com/mkulima_mbunifu)

